# CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY

# MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA

# MWONGOZO KWA SOKO LA KUKUZA UJASIRIAMALI NA KAMPUNI KUPITIA MASOKO YA MITAJI TANZANIA

## Yaliyomo


1. Utangulizi ........................................................................................................2
2. Umuhimu wa Soko la Kukuza Ujasiriamali ...............................................2
3. Mabadiliko katika muundo wa soko............................................................3
4. Faida za Soko la Kukuza Ujasiriamali .........................................................4
5. Masharti ya kuorodhesha kampuni kwenye Soko la Kukuza Ujasiriamali (EGM) ...............................................................................5
6. Taratibu za kuorodheshwa...........................................................................6
7. Majukumu ya wataalamu tofauti ...............................................................6
8. Masharti ya kuteuliwa kama Mshauri Mteule...........................................8
9. Gharama za kushiriki kwenye soko la kukuza ujasiriamali .................8
10. Orodha ya Madalali wa Soko la Hisa la Dar es Salaam..............................................................................................10
11. Orodha ya Washauri wa Uwekezaji....................................................11

## MWONGOZO KWA SOKO LA KUKUZA UJASIRIAMALI NA KAMPUNI KUPITIA MASOKO YA MITAJI TANZANIA

## 1. Utangulizi

Katika juhudi za kuendeleza soko la mitaji, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji nchini ilifanya utafiti kuhusiana na muundo wa masoko ya mitaji unaofaa kwa mazingira ya hapa nchini Tanzania. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha haja ya kufanya marekebisho kwenye mfumo wa masoko ya mitaji kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na kusaidia utekelezaji wa sera za taifa zinazolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi. Miongoni mwa sera hizo ni mpango wa kuendeleza makampuni madogo na ya kati kwa kuzingatia umuhimu wa makampuni haya kwenye uchumi wa nchi. Pia serikali inatekeleza mipango mingine ya maboresho kwa uchumi wa nchi kama vile mpango wa kuratibisha biashara (MKURABITA) na mkakati wa kukuza uchumi Zanzibar (MKUZA).

Ili kutekeleza sera hizo na nyinginezo, ilibainika kuwa ni muhimu kuwa na sehemu ya soko la hisa ambalo litahusika na makampuni ya aina fulani yenye mchango mkubwa katika juhudi za kukuza uchumi wa nchi yetu. Makampuni haya yanahitaji soko maalum zaidi ya safu ya soko kuu la sasa, ambalo litayawezesha kupata mitaji na kuchangia kwenye uchumi wetu. Mamlaka (CMSA) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) wamedhamiria kuanzisha safu ya soko maalum la kusaidia kukuza ujasiriamali ambalo litayawezesha makampuni madogo na ya kati kuweza kupata mtaji kwa ajili ya kukuza biashara na uzalishaji.

## 2. Umuhimu wa Soko la Kukuza Ujasiriamali

Soko la kukuza ujasiriamali limewalenga wajasiriamali na biashara za kati na ndogo. Ubinafsishaji na kufuata sera za soko huria kumesaidia kukua kwa haraka kwa sekta binafsi ambayo ni pamoja na makampuni madogo na yale ya kati. Hata hivyo tafiti za sera za serikali na utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana nchini zilibaini kuwa mojawapo ya vizuizi vya kukua kwa sekta binafsi hususan biashara ndogo na za kati hapa Tanzania ni ukosefu wa mtaji.

Mpango wa kurasimisha mali unaotekelezwa na serikali ya Tanzania bara na ule wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa Zanzibar una lengo la kuweka mazingira mazuri ya kukua kwa ujasiriamali kupitia biashara mpya na kuimarisha biashara zilizopo. Mipango hii inalenga kuwawezesha wenye mapato madogo kupata mitaji kwa kutumia mali zao nyingine kama vile nyumba na ardhi. Lengo jingine la mikakati hii ni kuwezesha Watanzania kushiriki kwenye masoko ya mitaji. Urahisi wa kushiriki kwenye masoko ya mitaji kutasaidia makampuni kuanza kushiriki kwenye uchumi wa nchi kwa uwazi zaidi na hivyo kuingia kwenye mfumo wa uchumi ulio rasmi. Mahitaji ya soko kuu yanazuia ushiriki wa makampuni madogo na hivyo kushindwa kufaidika na masoko ya mitaji nchini.

Benki za biashara haziwezi kukidhi haja ya kutoa mtaji kwa kampuni ndogo na za kati kutokana na makampuni hayo kutokuwa na mali za kutosha kuweka kama rehani na viwango vikubwa vya riba. Hali hiyo imepelekea mikopo ya benki kuwa michache kwa makampuni haya, mikopo kuwa ghali (riba inayotozwa na mabenki ni kubwa) na ya muda mfupi na yenye masharti magumu. Kwa ujumla, MKURABITA unategemewa kubadilisha mfumo wa dhamana zinazohitajika na benki kwa ajili ya kupata mkopo. Kuanzishwa kwa soko la kukuza ujasiriamali kutaleta ushindani baina ya mabenki na soko la hisa na kutoa nafasi ya kupata mitaji kwa biashara ndogondogo.

Sababu nyingine ya kuwa na soko la kukuza ujasiriamali ni kusaidia kukua kwa masoko ya mitaji. Soko hili linategemewa kuleta mwamko mpya kwenye masoko ya mitaji na kufanya soko la hisa kuchangamka kutokana na kuongezeka kwa makampuni yaliyoorodheshwa. Kuwepo kwa makampuni zaidi kwenye soko la hisa kunamwongezea mwekezaji fursa za kuwekeza kwenye makampuni mengi zaidi na hivyo kumsaidia kuanzisha mseto wa uwekezaji. Soko hili litachangia kuongezeka kwa uwekaji wa akiba hapa nchini.

## 3. Mabadiliko Katika Muundo wa Soko

Baada ya kuwa na haja ya kubadilisha muundo wa masoko ya mitaji hapa Tanzania, Mamlaka ilitafakari njia mbalimbali za kurekebisha mfumo wa masoko ya mitaji. Njia zilizofikiriwa ni pamoja na kuendeleza biashara ya mezani (OTC) au kuanzisha soko mbadala. Utafiti uliofanywa na Mamlaka (CMSA) ulibainisha kuwepo kwa mfumo wa soko lenye safu ya masoko mawili: soko kuu na soko mbadala. Uzoefu wa nchi zingine pia ulionyesha kupendelea kuwa na mfumo kama huu. Utafiti ulibaini kuwa kwenye nchi zingine, biashara ya mezani haijaendelea na imekuwa na vikwazo vingi katika maendeleo ya masoko ya mitaji. Mamlaka ilifikia uamuzi kuwa biashara ya mezani (OTC) haifai kwa kuendeleza masoko ya mitaji hapa nchini. Baadhi ya makampuni pia yalipinga kuwepo kwa biashara hii na kupendekeza kuwa na soko mbadala. Maendeleo ya biashara hii isiyo rasmi yamekuwa hafifu kutokana na matatizo yake ambayo ni pamoja na kukosa uwazi, wizi na uongozi mbovu wa masoko hayo. Jambo hili limepunguza imani ya wawekezaji na makampuni kwenye soko hili.

Kutokana na matatizo hayo hapo juu, ilibainika kuwa soko mbadala ambalo litasaidia kukuza ujasiriamali lingekuwa ndio ufumbuzi wa makampuni yaliyoshindwa kufikia viwango vya kuorodheshwa kwenye safu ya soko kuu. Uamuzi ulipitishwa kuwa soko la hisa liwe na masoko mawili: soko kuu na soko la kukuza ujasiriamali. Soko la kukuza ujasiriamali litakuwa na masharti nafuu kuliko soko kuu. Soko hili lina hatari zaidi kuliko soko kuu kutokana na kuorodhesha makampuni mapya na madogo ambayo hayana uzoefu mkubwa. Soko la kukuza ujasiriamali

linategemewa kuyaandaa makampuni kuingia kwenye soko kuu baada ya kukua na kukidhi masharti ya soko kuu.

## 4. Faida za Soko la Kukuza Ujasiriamali

### 4.1. Watoaji dhamana

4.1.1. Soko hili linatoa nafasi kwa makampuni ambayo yasingeweza kupata mtaji kupitia soko kuu;

4.1.2. Kuyawezesha makampuni yenye mawazo mazuri ya biashara kupata mtaji unaotakiwa kwa ajili ya kujipanua;

4.1.3. Kuongezea makampuni wigo wa kupata mtaji;

4.1.4. Makampuni yatakayotaka kuongeza mtaji baada ya kuwa yameorodheshwa kwenye soko hili yatakuwa kwenye nafasi ya kujua kwa uhakika bei ya hisa mpya;

4.1.5. Miradi mipya ambayo isingewezekana kutekelezwa kwa kukosa mtaji itaweza kutekelezwa;

4.1.6. Soko hili lina mfumo unaoyasaidia makampuni ambayo hapo baadae yanaweza kufikia kiwango cha kuorodheshwa kwenye soko kuu kupanga mipango yake vizuri tangu wazo la kufanya biashara yenye uwezekano wa kutoa faida ya kuridhisha linapozaliwa.

### 4.2. Wawekezaji

4.2.1. Wawekezaji watakuwa na uchaguzi mpana wa mahali pa kuwekeza fedha zao;

4.2.2. Soko hili linaweza kutumika kama njia ya kutawanya uwezekano wa kupata hasara (risk diversification) ;

4.2.3. Wawekezaji watapata urahisi wa kuuza hisa zao pale wanapohitaji; na

4.2.4. Wawekezaji kwenye hisa za makampuni yaliyojiorodhesha kwenye soko hili wataweza kutumia hisa zao kama rehani pale watakapokuwa wanataka mikopo kwenye benki kwani thamani ya hisa hizo itakuwa inajulikana.

### 4.3. Uchumi

4.3.1. Soko hili litasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji - kuingia kwenye masoko ya mitaji kupitia soko hili bado kunahitaji kampuni kufuata masharti ambayo yanawezesha mamlaka na umma kwa ujumla kuangalia mwenendo wa kampuni. Hili linasaidia kuongezeka uwazi kwenye shughuli za kampuni;

4.3.2. Kodi ya Serikali itaongezeka kutokana na kuongezeka kwa uwazi kwenye makampuni yaliyoko kwenye soko hili – makampuni yaliyo kwenye masoko ya mitaji kwa kawaida yana uwazi wa

kutosha na hivyo kuwa na fursa finyu sana ya kukwepa kodi. Hii inategemewa kuchangia katika ulipaji wa kodi serikalini;

4.3.3. Litasaidia utekelezaji wa sera za Serikali kuhusiana na makampuni madogo na ya kati na uwezeshaji kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania –MKUKUTA, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania –MKURABITA na Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar-MKUZA. Mipango yote hii inahitaji mitaji na masoko ya mitaji yatasaidia utekelezaji wake;

4.3.4. Soko hili litachangia kwenye ajira kutokana na kupanuka kwa utendaji wa makampuni haya baada ya kupata mitaji. Ajira zitaongezeka kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi;

4.3.5. Soko hili litachangia uwezeshaji wa watanzania kiuchumi kwa kuwezesha mtaji kupatikana na hivyo kuchangia ukuaji wa sekta binafsi itakayowezesha watanzania wengi zaidi kushiriki kwenye uchumi wa nchi yao.

## 5. Masharti ya kuorodhesha kampuni kwenye Soko la Kukuza Ujasiriamali (EGM)

Yafuatayo ni masharti kwa kampuni inayoomba kuuza hisa na kuorodheshwa chini ya EGM:

**5.1.** Lazima iwe imesajiliwa kama kampuni ya umma chini ya Sheria ya makampuni;

**5.2.** Hakuna kiwango maalum cha mtaji kinachotakiwa;

**5.3.** Historia ya utendaji kazi haihitajiki;

**5.4.** Historia ya upatikanaji faida haihitajiki;

**5.5.** Kama kampuni haitakuwa na historia ya utendaji kazi, waanzilishi hawataruhusiwa kuuza hisa zao katika miaka mitatu ya mwanzo baada ya kampuni kuwa imeorodheshwa;

**5.6.** Kampuni lazima iwe na Mshauri Mteule;

**5.7.** Lazima iwe na mpango wa biashara wa miaka mitano na taarifa ya ufundi ya kujitegemea iliyotayarishwa na Mshauri Mteule kuhusiana na matarajio ya upatikanaji faida;

**5.8.** Kiwango cha chini cha wanahisa ni 300;

**5.9.** Umiliki wa umma kwenye kampuni iliyo kwenye soko hili unatakiwa usipungue 20% ya hisa zilizotolewa;

**5.10.** Lazima kutengeneza Waraka wa Matarajio na upitishwe na Mamlaka;

**5.11.** Waraka wa Matarajio kwa Ufupi uwekwe kwenye magazeti;

**5.12.** Lazima kuwe na Kamati ya Ukaguzi kama mwongozo wa utawala bora wa makampuni unavyotaka;

**5.13.** Katiba na Waraka wa kuanzishwa kwa kampuni inabidi itamke ulazima wa kufuata misingi ya utawala bora wa makampuni.

## 6. Taratibu za kuorodheshwa

Kampuni ambayo imetimiza masharti ya mwanzo ya kuorodheshwa inabidi ifuate utaratibu ufuatao:

**6.1.** Kuteua timu ya wataalam washauri (consultants) kuiandaa kampuni kwa ajili kuuza hisa kwa umma na kuorodhesha hisa hizo kwenye soko la hisa;

**6.2.** Kuteua Mshauri Mteule kuisimamia kampuni tangu wazo la kutafuta mtaji linapokuja hadi kuirodhesha kwenye soko la kukuza ujasiriamali;

**6.3.** Kutengeneza Waraka wa Matarajio kwa ajili ya kuuza hisa kwa umma kama inavyotakiwa na kanuni za Mamlaka na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana;

**6.4.** Kampuni inabidi ibakie na Mshauri Mteule kwa kipindi chote ambacho kampuni itakuwa imesajiliwa kwenye soko;

**6.5.** Inabidi kuwasilisha Mamlaka (CMSA) na soko la hisa (DSE) maombi ya kuuza hisa na kuorodheshwa kwenye soko la hisa; na

**6.6.** Kupitishwa kwa Waraka wa Matarajio kunaiwezesha kampuni kuanza kuuza hisa zake kwa umma kama ilivyoelezwa hapo juu kwenye soko la awali.

## 7. Majukumu ya Wataalamu Tofauti

### 7.1. Mshauri Mteule

Hii ni aina mpya ya mshauri katika matoleo ya kwanza ya hisa. Mshauri mteule atafanya kazi kwenye Soko la kukuza ujasiriamali tu. Kwasababu baadhi ya makampuni yatakayoorodheshwa chini ya soko hili yatakuwa ni yale yenye kuanza biashara mpya. Kwa ajili hiyo, wajibu wa Mshauri Mteule utakuwa ni kutoa ushauri wa kitaalam wakati wote kwa makampuni kama haya ambayo yanaweza kuwa na mawazo mazuri ya biashara lakini yakawa na tatizo la mtaji. Kampuni kama hizi zinategemewa kutumia masoko ya mitaji kupata mtaji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kijasiriamali kwa kujiorodhesha kwenye soko la kukuza ujasiriamali. Baadhi ya kampuni hizi zinaweza kuwa ni za kundi la makampuni madogo na ya kati zikihitaji mtaji. Mshauri Mteule ataiongoza kampuni kwa ajili ya mambo yote yanayohusiana na kuorodheshwa kwenye soko, kutayarisha Waraka wa Matarajio na kuiongoza kampuni kutimiza masharti ya kudumu ya soko kwa kipindi chote ambacho kampuni itaendelea kuwa imeorodheshwa kwenye soko la hisa.

Makampuni ambayo yanapenda kujiorodhesha katika soko la kukuza ujasiriamali yataruhusiwa tu kufanya hivyo yatakapokuwa yameteua Mshauri Mteule. Uteuzi wa Mshauri Mteule utakuwa ni sharti la kampuni kuruhusiwa kujiorodhesha katika soko hili maalum. Mshauri Mteule atawajibika iwapo kampuni anayoishauri itafanya vibaya kibiashara na ikathibitika kuwa kushindwa huko kumetokana na uongozi wa kampuni hiyo kuzembea.

## 7.2. Washauri wengine

**Mshauri mkuu** – hawa ni wataalamu wanaoandaa waraka wa matarajio, kutathminisha kampuni na kuwasimamia washauri wengine wote.

**Dalali kiongozi** – hawa ni wataalam wanaounganisha kampuni na soko la hisa (DSE) na Mamlaka (CMSA) wakati wa kupeleka maombi ya kuorodhesha makampuni kwenye soko la hisa.

**Wahasibu** – hawa ni wataalamu wa uhasibu wanaopitia makisio ya kampuni na kushauri kuwa yameandaliwa kama inavyoelezwa kwenye waraka wa matarajio. Wahasibu wanaangalia matarajio ya kampuni kama yalivyobainishwa kwenye waraka wa matarajio ikiwa ni pamoja na vigezo vilivyotumika kuandaa matarajio hayo. Wahasibu hawa wanatoa taarifa isiyopendelea kuhusu matarajio ili kujenga imani ya wawekezaji. Kwa kawaida, mkaguzi wa mahesabu ya kampuni hawezi kuandaa ripoti ya wahasibu kwa ajili ya kuiweka kwenye waraka wa matarajio. Kutofautisha majukumu haya kunasaidia kuongeza uhakika wa taarifa kuhusu kampuni. Pia bodi ya taifa ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu imetoa mwongozo wa kuzuia kufanyika kwa kazi hii na mkaguzi wa hesabu.

**Wanasheria** – hawa ni wataalam wa sheria wanaotoa maoni kuhusu matakwa ya kisheria ya kampuni. Wanasheria wanahusika kuishauri kampuni kutekeleza masharti yote ya kuorodheshwa kwenye soko la hisa ikiwa ni pamoja na kuandaa waraka wa matarajio kulingana na sheria ya masoko ya mitaji na dhamana. Wanasheria pia wanaandaa mikataba ya washauri wengine na kampuni kwa niaba ya kampuni na kutoa maoni ya kisheria kuhusu kampuni, kuandikishwa kwake, umiliki wa mali na rasilimali pamoja na madai yoyote dhidi ya kampuni (kama yapo).

**Wapokeaji/ mawakala wa fedha kwenye mauzo ya hisa –** uuzaji wa hisa kwa umma huhitaji ushiriki wa taasisi mbalimbali zitakazokuwa zinapokea maombi ya kununua hisa kutoka kwa wawekezaji. Kanuni za utoaji hisa kwa umma huhitaji kampuni kuteua wapokeaji wa fedha kwenye mauzo ya hisa. Mapokezi yanaratibiwa na benki teule. Benki hii ndiyo itakayokusanya fedha zote na kuziwakilisha kwa kampuni. Benki hii pia inatakiwa kuhakikisha kuwa fedha yote iliyopokelewa pamoja na fomu za maombi zinapokelewa kulingana na mkataba wa huduma baina ya banki teule na wapokeaji wengine. Benki teule huratibu mawakala wengine ambao ni pamoja na benki nyingine na madalali wa soko la hisa,

shirika la posta Tanzania pamoja na taasisi nyinginezo zinazoweza kuteuliwa kushiriki kwenye mauzo ya hisa kwa umma.

## 8. Masharti ya kuteuliwa kama Mshauri Mteule

Mshauri Mteule kama ilivyokwisha elezwa ni aina mpya ya mshauri wa uwekezaji katika soko la mitaji Tanzania. Mshauri Mteule anatakiwa kuendelea kuishauri kampuni kwa kipindi chote ambacho kampuni hiyo itakuwa imeorodheshwa labda kama kampuni hiyo itaondolewa kwenye orodha ya makampuni yaliyoorodheshwa au kukua na kufikia hatua ya kuwa kwenye soko kuu. Masharti yanayotakiwa kutimizwa na kampuni inayotaka kuteuliwa kuwa Mshauri Mteule ni kama haya yafuatayo:

**8.1.** Lazima iwe ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria ya makampuni

**8.2.** Inabidi iwe na wataalamu wa kutosha waliopewa leseni na Mamlaka;

**8.3.** Inatakiwa iwe na mtaji wa kutosha kama itakavyokuwa imeelezwa na Mamlaka.

## 9. Gharama za kushiriki kwenye soko la kukuza ujasiriamali

### 9.1. Ada ya Kupitia Waraka wa Matarajio (CMSA)

| **Thamani ya Hisa** | **Ada** |
|---|---|
| TZS bilioni 1 au chini yake | TZS 1,000,000 |
| Kati ya TZS bilioni 1 na bilioni 5 | TZS milioni 1 ongeza 0.1% ya kiasi kinachozidi TZS bilioni 1 |
| Kati ya TZS bilioni 5 na 10 | TZS milioni 5 ongeza 0.05% ya kiasi kinachozidi bilioni 5 |
| Zaidi ya TZS bilioni 10 | TZS milioni 7.5 ongeza 0.025% ya kiasi kinachozidi TZS bilioni 10 |

### 9.2. Ada ya kuorodheshwa DSE

| | |
|---|---|
| Ada ya mwanzo ya kujisajili | 0.1% ya thamani ya hisa zinazo orodheshwa (kiasi cha chini TZS milioni 1 na kiasi cha juu TZS milioni 10) |
| Ada ya kusajili hisa nyingine | 0.1% ya thamani ya hisa zinazoongezwa (kiasi cha chini TZS milioni 1 na kiasi cha juu TZS milioni 10) |
| Ada kwa kila mwaka | 0.025% ya thamani ya hisa (kiasi cha chini TZS milioni 1 na kiasi cha juu TZS milioni 10) |

## 10. Tahadhari

Uwekezaji kwenye masoko ya mitaji una uwezekano wa kupata hasara. Kampuni ambazo zinaorodheshwa kwenye soko hili ni za mashaka makubwa zaidi (high risk) kwa wawekezaji kwa sababu ya kutokuwa na historia ya utendaji na hivyo kuwa na uwezakano wa jambo lolote kutokea. Kwa kuzingatia hali hiyo wawekezaji katika soko hili wanategemewa kuwa makini pale wanapofanya uamuzi wa kuwekeza pesa zao kwa kuangalia mambo mbalimbali kuhusiana na kampuni. Kwa kawaida ni wawekezaji wenye uwezo wa kuchambua makampuni na kufanya maamuzi wanaotegemewa kuwa wawekezaji wakubwa katika soko hili. Kwa wale ambao hawana uwezo wa kuchambua makampuni wanashauriwa kuwasiliana na washauri wa uwekezaji kabla ya kuwekeza kwenye kampuni zilizosajiliwa chini ya soko hili.

*Kiambatisho 1*

## ORODHA YA MADALALI WA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM

**1. Rasilimali Ltd.**
Jengo la zamani la TACOSHIL Sokoine Drive, DSM
Simu: +255 22 211 1708
Faksi: +255 22 212 2883
Barua pepe: rasilimali@africaonline.co.tz

**2. Tanzania Securities Ltd.**
Ghorofa ya 7, IPS Building
Mtaa wa Samora na Azikiwe, DSM
Simu: +255 22 211 2807
Faksi: +255 22 211 2809
Barua pepe: tsl@muchs.ac.tz

**3. Solomon Stock Brokers Ltd.**
Ghorofa ya chini, PPF House
Mtaa wa Samora na Morogoro, DSM
Simu: +255 22 211 2874
Faksi: +255 22 213 1969
Barua pepe: solomon@intafrica.com

**4. Vertex International Securities Ltd.**
Jengo la Annex – Zambia High Commission
Mtaa wa Sokoine na Ohio, DSM
Simu: +255 22 211 0392
Faksi: +255 22 211 0387
Barua pepe: vertex@intafrica.com

5. **Orbit Securities Co. Ltd.**
Ghorofa ya 3, Twiga house
Mtaa wa Samora, DSM
Simu: +255 22 211 1758
Faksi: +255 22 211 3067
Barua pepe: orbit@orbit.co.tz

**6. Core Securities Co. Ltd.**
Ground Floor, Twiga house
Samora Avenue, DSM
Tel: +255 22 2123103
Fax: +255 22 2182521
Email: info”@coresecurities.co.tz

*Kiambatisho 2*

**Licensed Investment Advisers (Washauri wa Uwekezaji)**

1. **Orbit Securities Company Limited**

3rd Floor, Twiga House, Samora Avenue
P.O.Box 70254 Dar es Salaam
Tel: 255 (22) 2111758
Fax: 255 (22) 2113067
E-mail: orbit-sec@raha.com

2. **Tanzania Securities Limited**

7th Floor, IPS Building, Samora Avenue / Azikiwe Street
P.O.Box 9821 Dar es Salaam
Tel: 255 (22) 21 12807
Fax: 255 (22) 21 12809
E-mail: tsl@muchs.ac.tz

3. **Standard Chartered Bank Tanzania Limited**

International House, Shaaban Robert / Garden Avenue
P.O.Box 9011 Dar es Salaam
Tel: 255 (22) 2122160 / 2122162
Fax: 255 (22) 2122089

4. **Rasilimali Limited**

Tacoshili Building, Sokoine Drive
P.O. Box 9373 Dar es Salaam
Tel: 255 - 22 - 2111711 / 255 (0) 744 777818
Fax: 255 - 22 - 2113438

5. **Consultants for Resources Evaluation Limited**

Ground Floor, Twiga Building Samora Avenue
P.o. Box 23227 Dar es Salaam
Tel: 255 - 22 - 2125147
Fax: 255 - 22 - 2122562
Email: core@cats-net.com

6. **Unit Trust of Tanzania**

3rd Floor, Sukari House Sokoine Drive / Ohio Street
P.O. Box 14825 Dar es Salaam
Tel: +255 22 212 250 I / 213 7592/ 212 8460 /61
Fax: +255 22 21 3 7593
Email: uwekezaji@utt-tz.org

Website: www.utt-tz.org

7. **Ernst &Young Advisory Services**

Utalii House, 36 Laibon Road Oysterbay
P.O.Box 2475 Dar es Salaam
Tel: +255 22 266 6853 / 266 7659
Fax: +255 22 266 6869
Email: EYAS@tz.ey.comguarantee@raha.com

8. **Choice Capital Management Company Ltd.**

5th Floor, NIC Life House, Wing B Sokoine Drive/ Ohio Street
P.0. Box 61269 Dar es Salaam
Tel: +255 22 213 3997
Website: www.choicecapitalmanagement.com

9. **Commercial Bank of Africa (Tanzania) Limited**

Amani Place, Ohio Street,
P.O. Box 9640, Dar es Salaam
Tel. +255 22 2130113
Fax: +255 22 2130116
E-mail: info@cba.co.tz
Website: www.cba.co.tz

10. **FTC Consultants Limited**

2nd Floor, Osman Towers Zanaki Street
P.O. Box 22731 Dar es Salaam
Tel: +255 22 211 5251 / 2 / 3
Fax: +255 22 213 0519
Email: info@mbn.co.tz

11. **Exim Advisory Services Ltd.**

8th Floor, Office Academy Scheme Building, Azikiwe Street
P.0. Box 3219 Dar es Salaam
Tel: +255 22 213 4156
Fax: +255 22 213 4157
Website: www.eximadvisoryservices.com

**CAPITAL MARKETS AND SECURITIES AUTHORITY**

**MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA**

**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana**
**Ghorofa ya 6, Jengo la PPF Tower,**
**Makutano ya Mtaa wa Ohio na Garden,**
**S.L.P. 75713 Dar es Salaam,**
**Simu: +255 22 2114959 / 61**
**Faksi: +255 22 2113846**
**Barua pepe: info@cmsa-tz.org**
**Tovuti: www.cmsa-tz.org**